**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MWONGOZO WA MASHINDANO YA KITAIFA YA SAYANSI TEKNOLOJIA NA UBUNIFU (MAKISATU)

**2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaratibu Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ambayo yaliasisiwa mwaka 2019 kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA). Mashindano haya ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuimarisha na kuendeleza teknolojia na maarifa asilia ya ndani ili yaweze kuchangia katika uchumi wa nchi.

## 2.0 LENGO LA MASHINDANO

Lengo la MAKISATU ni kuibua, kutambua, kuadhimisha, kujenga, kukuza na kuendeleza ubunifu wa Watanzania katika nyanja za Sayansi na Teknolojia ili kuchangia juhudi za maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Matokeo tarajiwa ya MAKISATU ni kukua kwa hamasa ya ubunifu katika nyanja ya sayansi na teknolojia; matumizi ya sayansi, teknolojia, na ubunifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii; kuendeleza ubunifu ili kufikia hatua ya ubiasharishaji; kuchochea ugunduzi na ubunifu wa kisayansi na teknolojia. MAKISATU yanafanyika kila mwaka.

**3.0** Kaulimbiu ya MAKISATU 2021 ni "**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Uchumi Endelevu"**

## 4.0 MAKUNDI YA WABUNIFU NA MFUMO WA UPATIKANAJI KATIKA MAKISATU 2021

Mashindano hayo yatashirikisha wabunifu kutoka makundi saba (7) ambayo ni:

i. Shule za Msingi;
ii. Shule za Sekondari;
iii. Vyuo vya Ufundi Stadi;
iv. Vyuo vya Kati;
v. Vyuo Vikuu;
vi. Taasisi za Utafiti na Maendeleo; na
vii. Mfumo usio Rasmi.

**Kundi la Shule za Msingi,** hushirikisha ubunifu kutoka kwa wanafunzi katika ngazi ya shule za msingi (Serikali na Binafsi);

**Kundi la Shule za Sekondari,** hushirikisha ubunifu kutoka kwa wanafunzi katika ngazi ya shule za sekondari (Serikali na Binafsi);

**Kundi la ufundi stadi,** hushirikisha ubunifu kutoka kwa wanachuo (wafanyakazi na wanafunzi) wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs);

**Kundi la Vyuo vya Kati**, hushirikisha ubunifu kutoka wanachuo (Wafanyazi na Wanafunzi) wa vyuo vya ufundi na mafunzo (Serikali na Binafsi);

**Kundi la Vyuo Vikuu**, hushirikisha ubunifu kutoka kwa wanachuo (Wafanyakazi na wanafunzi) wa vyuo vikuu (Serikali na Binafsi);

**Kundi la Utafiti na Maendeleo**, hushirikisha ubunifu kutoka kwa wafanyakazi wa Taasisi za Utafiti na Maendeleo (Serikali na Binafsi); na

**Kundi la Mfumo usio Rasmi,** hushirikisha ubunifu kutoka kwa wabunifu walio nje ya mfumo rasmi.

## 5.0 URATIBU WA MASHINDANO

Mashindano hayo yanaratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, ushiriki wa wabunifu unaratibiwa kwa makundi kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 1: Uratibu wa Mashindano

| Na. | KUNDI | MRATIBU | Anuani |
|---|---|---|---|
| 1 | Shule za Msingi | WyEST & TAMISEMI | makisatu@moe.go.tz |
| 2 | Shule za Sekondari | | |
| 3 | Vyuo vya Kati | DIT, NACTE | info@nacte.go.tz |
| 4 | Taasisi za Utafiti & Maendeleo | COSTECH | dg@costech.or.tz |
| 5 | Vyuo Vikuu | | |
| 6 | Ufundi Stadi | VETA | info@veta.go.tz |
| 7 | Mfumo usio Rasmi | | |

## 6.0 USAJILI WA KUSHIRIKI KATIKA MAKISATU

Maombi ya kushiriki katika mashindano kutoka kwa wabunifu yatafanyika kwa kutumia fomu namba WTF 7 (Kiambatisho-1) na kuwasilishwa kwa mratibu wa kundi husika kupitia barua pepe zilizotajwa katika jedwali Na. 1 au kwa kuwasilisha ana kwa ana katika ofisi husika. Pia, unaweza kuwasilisha maombi kwa njia ya mfumo wa kielektroniki kupitia wavuti www.makisatu.costech.or.tz. Kwa wabunifu ambao watakuwa na changamoto katika ujazaji wa fomu za usajili wapige simu namba 0754 520 176 au 0784 865 994 au barua pepe makisatu@moe.go.tz kwa ufafanuzi na msaada.

## 7.0 VIGEZO VYA USHIRIKI KATIKA MAKISATU

(i) Mshiriki lazima awe Mtanzania, pasipo kuzingatia kiwango cha elimu wala umri;
(ii) Ubunifu uwasilishwe na mbunifu husika;
(iii) Ubunifu unaofanywa na makundi au Taasisi, uwasilishwe kwa Jina la Taasisi au kama ni kundi la Wabunifu kwa Jina la kikundi chenye ubunifu husika;
(iv) Mbunifu mmoja anaruhusiwa kuwasilisha ubunifu zaidi ya mmoja;
(v) Mbunifu aliyeshiriki katika fainali za MAKISATU katika miaka iliyopita na hajakamilisha uendelezaji wa ubunifu uliofadhiliwa, hatoruhusiwa kushiriki katika mashindano ya mwaka unaofuata; na
(vi) Ubunifu ambao haukufika hatua ya fainali za MAKISATU katika mwaka uliopita unaruhusiwa.

## 8.0 UTARATIBU WA UENDESHAJI WA MAKISATU

(i) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itatangaza tarehe ya kuanza na kuhitimisha usajili wa ubunifu kwa mwaka husika;
(ii) Wabunifu watawasilisha maombi ya ushiriki kupitia kwa Taasisi zinazohusika na uratibu wa kundi;
(iii) Waratibu wa kila kundi watafanya tathmini ya mawasilisho na kuchagua ubunifu kumi bora (10) kwa kila kundi ambao utashiriki kwenye fainali ya Kitaifa;
(iv) Majaji watafanya tathmini ya kina kwa kila ubunifu katika hatua ya fainali za MAKISATU kwa kupitia mawasilisho, kufanya mahojiano na mbunifu na

kutathmini ubunifu, kisha utafanyika ulinganifu wa alama na kupata ubunifu mahiri tatu (3) kwa kila kundi utakaotunukiwa tuzo; na

(v) Ubunifu utakaoshiriki katika hatua ya fainali utaendelezwa kupitia utaratibu maalum ambao unaratibiwa na COSTECH.

**FOMU ITAKAYOTUMIKA KATIKA MAKISATU**

**Kiambatisho-1**

**MAOMBI YA USHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KITAIFA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU (WTF 7)**

1. Taarifa za Mwombaji

**Sehemu A: Ijazwe na Mwombaji binafsi**

Jina Kamili……………………………………………………

Anuani ………………………..……………………………....

Simu…………………………………………………………..

Taasisi ……………………………..…………………………..…

Makazi…………………………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa …………………………….……………..…

Barua pepe…………………………..…………………………

Uraia ………………………………………..……………………

Kiwango cha Elimu ……………………………………………..…

Taaluma ……………………..………………………………

Kazi ……………………………………...……………………

**Sehemu B: Ijazwe na Taasisi/Kikundi (*iwapo taasisi/kikundi kinaomba kushiriki katika MAKISATU 2021*)**

Jina Kamili…………………………………………………

Anuani ………………………..………………………………

Simu…………………………………………………………….

Barua pepe ……………………………..……………………….

Aina ya Taasisi …………………………………………...

Mahali Taasisi ilipo ………………………………………

Uga wa Umahiri ……………………………..………………

Namba ya usajili wa Taasisi …………………….……….

Aina ya Usajili ……………………………………...

2. Jina la Ubunifu/Ugunduzi/Maarifa Asilia: ………………….……………….

Eleza kwa ufupi kuhusu Ubunifu/Ugunduzi/Maarifa Asilia husika

…………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………

3. Je, umewahi kushiriki katika MAKISATU? Jibu NDIYO/HAPANA ……………………, kama NDIYO taja mwaka/miaka uliyoshiriki …………, jina la Ubunifu/Ugunduzi/Maarifa Asilia ……………………….……………… na hatua uliyofikia (awali, fainali na mshindi) …………………………………………

4. (i) Je, Ubunifu/Ugunduzi/Maarifa Asilia yako yanatatua changamoto zipi katika jamii?

   …………………………………………………………..……………………………

   ……………………………………………………………………………………………

   (ii) Kutokana na changamoto ulizoainisha hapo juu elezea kwa undani, ikiwa ni pamoja na kuambatisha vielelezo muhimu kama vile michoro muhimu, picha na maelezo mengine

   ……………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………………

5. (i) Elezea kwa kifupi ikiwa unafahamu kama ubunifu wako umewahi kufanywa na mtu mwingine ………………………………………………………………………………

   (ii) Je, ni kitu gani kipya katika ubunifu wako ukilinganisha na kile ambacho kilishafanyika? ……………………………………………………………………………..

6. Je, Ubunifu/Ugunduzi/Maarifa Asilia yamekamilika? Jibu NDIYO/HAPANA ……………………………….………………

   Kama jibu ni NDIYO, je, unatumika katika jamii? ……………………….

   Kama jibu ni HAPANA, elezea maboresho yanayohitajika ……………………………

   ………………………………………………………………………..

7. Je, Ugunduzi/Ubunifu/Maarifa asilia yamepata aina yoyote ya Hakimiliki?

   Jibu NDIYO/HAPANA ……………………..

   Kama jibu ni NDIYO, weka alama ya (  )

Hataza ……………………..…  Nembo ya Biashara ………

Hataza ndogo ……………...  Siri ya Kibiashara …………

Usanifu wa kiviwanda ……

Haki Miliki Dhihini ……..  Haki za Watafiti wa Mbegu za Mimea (PBR) ……….

8. Eleza umuhimu wa ubunifu/ugunduzi/ maarifa asilia yako:

   (i) Jinsi ulivyochangia au unavyoweza kuchangia katika kujenga au kuendeleza taaluma/weledi/umahiri?

   …………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………...……………………………………...

   (ii) Jinsi ulivyochangia au unavyoweza kuchangia kujenga maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi hapa nchini

   ……………………………………………………………………..…..………………….

   …………………………………………………………………………………………

9. Je, umeshirikiana na mtu mwingine katika ubunifu/ugunduzi/maarifa asilia hayo? Jibu NDIYO/HAPANA ……………………..

Kama NDIYO, eleza kwa kifupi.

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………..……………………………....

Maombi haya na taarifa nyingine zitumwe katika anuani zilizotajwa katika jedwali Na. 1.

Kwa mawasiliano na taarifa zaidi;
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P. 10,
DODOMA
Barua pepe: makisatu@moe.go.tz
Simu: 0754 520176 au 0784865994